



Juni 01, 2020

Gazeti la Reli | Toleo Namba 7 | Habari | Makala | Matukio | Elimu | Picha

WAZIRI MKUU ARIDHISHWA NA MAENDELEO YA MRADI WA UJENZI WA RELI YA KISASA - SGR



Na Mwandishi wetu TRC

Meneja Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR Morogoro - Makutupora - Singida Mhandisi Tito Matesh (kulia) akimuonesha Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Handaki namba tatu linaloendelea kujengwa Kilosa mkoani Morogoro hivi karibuni Mei, 2020.

Waziri mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa ameridhishwa na maendeleo ya mradi wa ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR alipotembelea awamu ya kwanza ya ujenzi kipande cha Dar es Salaam hadi Kilosa - Morogoro Mei, 2020.

Waziri mkuu amesema kuwa ni hatua kubwa sana iliyofanyika katika ujenzi wa mradi wa SGR ambapo kipande cha kwanza Dar es Salaam- Morogoro cha ujenzi umefikia asilimia zaidi ya asilimia 77.

“Nimeshuhudia mwenyewe kwa kupanda treni ya majaribio ya wahandisi ili nijiridhishe na ukaguzi wa njia na kiukweli nimeridhika” alisema Mhe. Majaliwa.

Aidha, Waziri Mkuu ameipongeza kampuni ambayo inasimamia ujenzi huo pamoja na kutoa pongezi za dhati kwa Shirika la Reli Tanzania - TRC kwa kufanya kazi usiku na mchana ili kuhakikisha mradi wa SGR unakamilika kwa uimara na kwa wakati unaostahili kulingana na masharti ya Serikali juu ya ujenzi huo. Pia Waziri Mkuu alitoa Shukrani zake kwa Mkurugenzi mkuu wa TRC pamoja na kamati nzima ya Bodi ya Shirika hilo kwa kutekeleza maagizo ya wizara pamoja na kutafuta kampuni nzuri kutoka Uturuki ya wakandarasi wa ujenzi wa reli ya kisasa Yapi Merkezi. “Kampuni hii imefanya kama Serikali ilivyotaka” aliongezea Mhe. Majaliwa.

WAZIRI MKUU ARIDHISHWA NA MAENDELEO YA MRADI WA UJENZI WA RELI YA KISASA - SGR


Na Mwandishi wetu TRC



Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa akieleza kuridhishwa kwake na maendeleo ya mradi wa SGR alipofanya ziara kukagua mradi huo Soga mkoani Pwani hivi karibuni Mei, 2020.



Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa (kati) akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa TRC Ndugu Masanja Kadogosa kuhusu maendeleo ya mradi wa SGR.



Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa akizungumza jambo na Mkurugenzi Mkuu wa TRC Ndugu Masanja Kadogosa ndani ya treni ya majaribio ya mradi wa SGR.

Waziri alivitaja vyanzo vitatu vya umeme ambavyo vitatumika katika uendeshaji wa treni ya umeme pindi itakapoanza uendeshaji na kusema kuwa vyanzo hivyo ni umeme kutoka Bwawa la Mwalimu Nyerere, umeme kutoka kidatu na Mtera na cha tatu ni umeme kutoka Kinyerezi kwa kutumia gesi inayotoka Mtwara.

“Nimetembea na nimeona nguzo za umeme 154 kati ya 160 zimeshasindikwa kwa awamu hii ya kwanza” alisema Mhe. Waziri.

Waziri Mkuu amependezwa na ujenzi wa vituo vya reli alipotembelea kituo cha reli cha Soga na kusema kuwa ni vituo vyenye viwango na vya kimataifa ambavyo vitazungukwa na huduma mbalimbali za kijamii.

Naye Naibu Waziri wa Uchukuzi na Mawasiliano Mhe. Atashasta Nditiye amesema kua hivi karibuni Serikali inatarajia kuja kuzindua safari kipande cha Dar es Salaam - Morogoro kwa kua awamu ya ujenzi katika kipande hicho kiko mbioni kukamilika.

Mhe. Nditiye amesema kuwa kuanza kutumika kwa reli hiyo ya kisasa kutaleta faida kubwa katika nchi ikiwemo ukuaji wa uchumi kwa kutumia mda mfupi na kukamilisha shughuli kwa haraka pamoja na jamii kufaidika katika kutokomeza hadha ya usafiri na kutumia treni ya mwendokasi.

Pia Mkurugenzi Mkuu wa TRC ndugu Masanja Kungu Kadogosa amesema kuwa changamoto nyingi zinajitokeza ila zinafanyiwa kazi kwa haraka kwa lengo la kupata ujenzi ulio bora na imara.

Hata hivyo Mkurugenzi Mkuu amesema kuwa ujenzi huo wa SGR unaenda kwa kasi kwa vipande vyote viwili ya Dar es Salaam - Morogoro na awamu ya pili ya Morogoro - Makutupora.

Juhudi za kuimarisha sekta ya miundombinu ya reli nchini zinatekelezwa na serikali ya Tanzania inayoongozwa na Dkt. John Pombe Magufuli kwa ajili ya watanzia. TRC inaendelea kuwakumbusha wananchi kuunga mkono juhudi zinazofanywa na Mhe. Rais Dkt. John Pombe Magufuli.

WANANCHI DODOMA WAMSHUKURU RAIS MAGUFULI KWA KUPATA FIDIA KUPISHA UJENZI WA SGR

Na Mwandishi wetu TRC



Wananchi jijini Dodoma wamemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli kwa kupata fidia baada ya maeneo yao kuwekwa katika orodha ya maeneo yanayopitiwa na mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa – SGR kipande cha Morogoro – Dodoma – Singida katika Kata za Ihumwa, Mkonze na Kikuyu Kusini mkoani Dodoma, hivi karibuni Mei 2020.

Zoezi hilo linahusisha fidia za nyumba na viwanja, jumla ya wananchi 2,604 wanatarajiwa kulipwa fidia yenye thamani ya zaidi ya Shilingi Bilioni 19 Dodoma wilaya ya Bahi na mkoani Singida ili kuwawezesha wananchi kupisha mradi. Baadhi ya wananchi wameonesha kufurahishwa na hatua hiyo na kuipongeza Serikali inayoongozwa na Rais Magufuli kwa kutimiza ahadi ya kuwalipa wananchi wote ambao maeneo yao yamepitiwa na mradi wa SGR.

Aidha, pamoja na pongezi hizo wananchi wa maeneo hayo wameahidi kuendelea kutoa ushirikiano ili kuhakikisha mradi huo unakamilika kwa wakati ili uweze kuwanufaisha katika shughuli zao za kila siku, pia wameridhishwa na tahadhari zinazochukuliwa na shirika katika kupambana na ugonjwa wa Corona.

Akiongea katika zoezi la ulipaji fidia moja kati ya wanaolipwa fidia Bwana Geogre Massawe amesema kuwa "sikutegemea kama Serikali ingelipa stahiki zao mapema, si kama walivyokuwa wakidhani maana maneno yalikuwa mengi kweli hii ni serikali ya awamu ya tano haibabai shwi wala haitetereki".

Bwana Masumbuko Mhagama mkazi wa Muungano B amesema kuwa Shirika la Reli Tanzania limetoa ushirikiano mkubwa sana katika zoezi hili kwani wamekuwa wakiwasikiliza na kutatua changamoto wana-zokutana nazo katika maeneo hayo yaliyochukuliwa.

Halikadhalika Ofisa kutoka Reli anaye shughulika na Masuala ya Jamii Bi. Marry Machungwa amewatoa hofu wananchi na kuwataka kuripoti endapo kuna changamoto za kijamii zinazowakabili wawe wazi kuwaelezea kwani wapo kwa ajili ya kutatua changamoto hizo.

Pia Shirika limetoa rai kwa wananchi wanaolipwa fedha zao kuangalia kama wameridhika na tathimini hiyo au kama hawajaridhika wanaweza wakaandika barua kwa TRC ili kuweza kuangalia tena suala hilo.

Mkuu wa Wilaya ya Kaliua azishauri taasisi zinazosimamia Miundombinu kuiga utendaji kazi wa TRC

Na Mwandishi wetu TRC



Mkuu wa wilaya ya Kaliua Bw. Abel Busalama azishauri taasisi zinazosimamia miundombinu kuiga utendaji kazi wa Shirika la Reli Tanzania - TRC ili kuweza kujifunza mbinu zinazotumika katika ukarabati wa miundombinu yake kutokana na kazi nzuri waliyoifanya hadi kukamilisha ujenzi wa tuta la reli katika mto Ugala na kurejesha huduma za usafiri wa treni kati ya mikoa ya Tabora na Katavi hivi karibuni Mei, 2020.

Daraja la reli katika mto Ugala River linalounganisha mikoa ya Tabora na Katavi lilikatika kufuatia maji yaliyofurika katika mto Ugala na kusomba sehemu ya tuta la reli lenye urefu wa zaidi ya mita 120 na kupelekea kusitishwa kwa safari za treni kwa takribani mwezi mmoja.

Mhe. Busalama alisema kuwa uzoefu huo wa kujenga tuta la reli ndani ya maji ni wa hali ya juu ambao umefanywa na wahandisi wa TRC kwa kuwa baadhi ya sehemu ya mto huo kuwa na kina kirefu cha maji takribani mita kumi ambapo ilihitaji umakini na ustadi katika kufanikisha kazi hiiyo.

“Teknolojia hiyo ya ‘Gabion’ iliyotumika, shirika lolote linaweza kuitumia katika kujenga na kukarabati miundombinu sio ya reli pekee hata ya barabara” alisema Mhe. Busalama.

Meneja Matengenezo TRC Mhandisi Machibya Masanja alisema kuwa viongozi wanatakiwa wawaamini wahandisi wa Tanzania katika nyanja mbalimbali za ujenzi na ukarabati wa miundombinu pamoja na kuwa na mitambo ya uhakika ya kufanyia kazi za ujenzi.

“Ukisha muaminisha mtu kuwa anaweza atafanikiwa” alisema Mhandisi Machibya, pia aliongezea kwa kusema “Sisi tumefanya kazi kama wahandisi kurejesha njia na kukarabati hili tuta”

Mkuu wa Wilaya ya Mpanda Mhe. Lilian Mtinga alisema kuwa Mkoa wa Katavi unategemea usafiri wa reli kwa asilimia kubwa kusafirisha mizigo pamoja na vyakula kupeleka katika kanda ya ziwa pamoja na kanda ya kati.

Aidha Mhe. Lilian aliongea kwa kusema kuwa wananchi wamefurahishwa na juhudi zilizofanya na Serikali ya awamu ya tano kwa kuwawezesha Shirika la Reli kusimamia miundombinu ya Reli na kujivunia kuona tuta hilo katika mto Ugala limekarabatiwa na wahandisi kutoka ndani ya nchi.

MAONI YA WADAU MKOANI DODOMA

Kiukweli Tunamshukuru sana Rais Magufuli kwa hili la kutupatia hundi zetu kwa wakati stahiki kabisa kwani hatukutegemea kuipata haki yetu kwa haraka ukiangalia na hili janga la Corona limeingilia kati ila zimeonekana jitihada za kujikinga na kuendelea na zoezi kusudi kila mfidiwa apate haki yake.
Mazengo H. Mazengo kutoka Chidachi, Dodoma



Utoaji huu wa hundi kwa wakati umetufanya wananchi tuendeleo kuamini kuwa serikali ya awamu ya tano inajali wanyonge na naamini watu watafanya vitu vya msingi kupitia haya mapato waliyopata pamoja na wanakijiji wengi kujenga nyumba za kisasa.

Munubi E. Neke kutoka Miganga, Dodoma

Tunaisubiri kwa hamu reli ya kisasa ikamilike kwani italeta faida kubwa katika nchi ya Tanzania hususani kwa Mkoa wetu wa Dodoma naamini mzunguko wa biashara utaongezeka kwa wingi kwa kuwa watu watasafirisha bidhaa kwa haraka na urahisi yaani sitaamini kama ntatoka Dodoma hadi Dar es Salaam kwa muda wa saa tatu.

Mathias J. Urio kutoka Dodoma



Usafiri wa Reli ni mzuri sana na tumetoka nao mbali, na uzee wangu huu najua faida ya kutumia njia ya reli hivyo hii mpya ya kisasa ikianza uchumi wa nchi utazidi kuwa mkubwa na tunaona ujenzi unavyopamba moto yaani serikali inafanya vizuri.

Charles E. Nyaulingo kutoka Msangalalee, Dodoma

MAONI YA WADAU MKOANI MOROGORO

Mimi hua napenda kufuatilia maendeleo ya miundombinu ya reli na naona ujenzi hasa wa reli hii mpya ya kisasa unavyokwenda kasi kama kwenye kipindi cha reli na matukio walionyesha mahandaki wilayani kilosa ambayo bado kidogo tuu kukamilika, hongereni sana shirika la reli na serikali kiujumla.
Martina Anselimo kutoka Kilosa, Morogoro



Katika mkoa wetu huu wa Morogoro tunajionea wenyewe njia za juu za reli japokua bado ziko mbioni kumalizika ila zitaleta manufaa makubwa na kizuri zaidi zimetengwa na barabara za kawaida na treni itapita juu hii itaondoa sana hadha ya usafiri.
Salum Ramadhani kutoka Morogoro

Kwa upande wangu naomba serikali iangalie hili suala la treni ya mwendokasi na upande wa kwetu kule magharibi Kigoma wananchi watafurahi sana sababu washazoea kutumia treni za kawaida sasa yakienda mageuzi ya treni ya umeme utakua unatumika mda mchache mno.

Zulfa Shirima kutoka Morogoro



Serikali yetu ya sasa iko vizuri sana wananchi tunayaona maendeleo kwa macho na sio maneno yaani reli hii inayojengwa imenyooka na nguzo za umeme zimeshaweka sehemu nyingi tumeziona na tunaipongeza na kumpongeza Rais wetu Magufuli.
Robert Damian kutoka Morogoro

Na Mpiga Picha Wetu TRC



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa akisalimiana na baadhi ya viongozi alipowasili katika Stesheni ya Soga kukagua mradi wa SGR mkoani Pwani hivi karibuni Mei, 2020



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa (kati) akitembea kuelekea eneo ambalo Handaki namba mbili lina-jengwa Kilosa mkoani Morogoro hivi karibuni Mei 2020.



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa (kulia) akijadili jambo na Waziri wa Nishati na Madini Mhe. Medard Kalemani (kushoto) pamoja na baadhi ya viongozi (hawapo pichani) katika treni ya uhandisi wakati wa ziara kukagua mradi wa SGR hivi karibuni Mei, 2020.



Kaimu Mkurugenzi wa Kampuni ya Yapi Merkezi Bwana Erdem Arioglu (kulia) akimuelezea Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa kuhusu maendeleo ya mradi wa SGR mkoani Pwani, hivi karibuni Mei 2020.



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa (kulia) akishuka kutoka ndani ya treni ya majaribio ya mkandarasi katika Stesheni ya Soga mkoani Pwani hivi karibuni Mei 2020.



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa (kulia) akizungumza na waandishi wa habari mara baada ya kushuka kutoka ndani ya treni ya majaribio ya mkandarasi katika Stesheni ya Soga mkoani Pwani hivi karibuni Mei 2020.

Na Mpiga Picha Wetu TRC



Maafisa kutoka Shirika la Reli Tanzania wakiwahudumia wananchi wa Mtaa wa Image mkoani Dodoma walipofika kwa ajili ya kupokea hundi za fidia mkoani Dodoma hivi karibuni Mei, 2020.



Bwana Cyprian Majura Musiba (kulia) akitia saini katika fomu wakati wa zoezi la ulipaji fidia ili aweze kupata Hundi ya malipo ya fidia kwa ajili ya kupisha Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR mkoani Dodoma hivi karibuni 2020.



Maafisa kutoka Benki ya Taifa ya Biashara - NBC (kulia) wakiwahudumia wananchi mkoani Dodoma wakati wa zoezi la ulipaji fidia hivi karibuni Mei, 2020.



Afisa Uhasibu kutoka TRC Bwana Yusuph Abdallah (kulia) akikagua nyaraka za Bwana Onesu Abel kabla ya kumkabidhi hundi ya malipo ya fidia katika mtaa wa Muungano 'B' Dodoma hivi karibuni Mei 2020.



Baadhi ya wananchi wa mtaa wa Muungano 'B' wakinawa mikono kwa maji na sabuni ikiwa ni tahadahri kujikinga na ugonjwa wa Corona, wakati wa zoezi la fidia mkoani Dodoma hivi karibuni Mei 2020.



Maafisa wa TRC wakiendelea kuwahudumia wananchi wa Kikuyu wakati wa zoezi la ulipaji fidia ili kupisha ujenzi wa reli ya Kisasa mkoani Dodoma hivi karibuni Mei, 2020.

TANGAZO

**SHIRIKA LA RELI TANZANIA – TRC
LINAWATANGAZIA WANANCHI
AMBAO MAENEO YAO YAMETWALIWA NA TRC
ILI KUPISHA MRADI WA UJENZI WA RELI YA
KISASA – SGR NDANI YA JIJI LA DODOMA,
WILAYA ZA BAHU NA MAKUTUPORA - SINGIDA
AMBAO HAWAKUWEPO WAKATI WA ZOEZI LA
UTHAMINI**

**WANANCHI HAO WANAOMBWA
KUANDIKISHA MAJINA YAO KWA
MAAFISA WATENDAJI WA MAENEO HUSIKA ILI
WAVEZE KUTAMBULIKA**

**ZOEZI LA UTHAMINI LITAANZA TAREHE
08 – 12 JUNI 2020 AMBAPO
WATHAMINI WATAPITA KUCHUKUA
TAARIFA ZA WAMILIKI WA MALI KATIKA
MAENEO HUSIKA ILI KUWEZESHA ULIPAJI
FIDIA**

**KWA TAARIFA ZAIDI WASILIANA NA
MAAFISA WATENDAJI KUHUSU SIKU RASMI
YA UTHAMINI KATIKA ENEO LAKO**

**UNAPOSIKIA TANGAZO HILI, MUARIFU NA
MWENZAKO**

**Kwa Maelezo zaidi piga Simu namba
0800110042 AU tuma ujumbe
kupitia Barua pepe info@trc.co.tz
na Mitandao ya kijamii**

**Facebook, Twitter, Instagram na LinkedIn
kwa jina @trailways**

RELI YETU | MAENDELEO YETU | TAIFA LETU

USHIRIKI WA MAKAMPUNI YA WAZAWA KATIKA UJENZI WA RELI YA KISASA - SGR

Na Mwandishi wetu TRC

Serikali katika nchi nyingi zinazoendelea zinakabiliwa na changamoto ya kuongezeka kwa mahitaji ya huduma mpya na bora za miundombinu ya usafirishaji na uchukuzi ili kuweza kuinua uchumi wa nchi na sekta nyingine wezeshi kupitia miundombinu.

Aidha fedha zinazopatikana ili kujenga miundombinu kutoka katika vyanzo vya ndani ya nchi mara nyingi huwa hazitoshelezi kutekeleza miradi mingi kwa wakati mmoja, lakini serikali ya Tanzania imeonesha uthubutu wa kujenga reli kwa kutumia fedha zake za ndani, kupitia uwekezaji huu mkubwa serikali ilichukua hatua ya kuhakikisha ushiriki wa kampuni za wazawa unapewa ki-paumbele ili kuiweesha kampuni hizo kupata uwezo na uzoefu katika utekelezaji wa miradi mikubwa.

Mradi huu wa reli ya kisasa – SGR utaunganisha maeneo ya kimkakati ya Tanzania pamoja na nchi jirani ambazo ni Rwanda, Burundi, Uganda, Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo, mradi huu unajengwa kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza. Tunaamini kuwa mradi huu reli ya kisasa SGR utaleta mapinduzi katika sekta ya usafirishaji na uchukuzi hasa katika kuchochea uchumi wa sekta mbalimbali na maendeleo ya watanzania katika shughuli za kiuchumi.

Ujenzi wa reli ya kisasa unajengwa na Mkandarasi kutoka nchini Uturuki YAPI MERKEZI huku akishirikiana na Kampuni za wazawa zaidi ya 600 na makampuni ya nje ya nchi 70, yote hayo yanafanya kazi mbalimbali kama wakandarasi wadogo, wakandarasi washauri wa mradi, watengenezaji na wasambazaji wa vifaa vya ujenzi vikiwemo nondo, mbao, na malighafi kama saruji, mafuta, mawe, mchanga na kokoto vinavyotumika wakati wa ujenzi.

Kampuni nyingi kutoka nchini zimejikita zaidi katika kutoa huduma mbalimbali ikiwemo bima, ujenzi, usafirishaji, usambazaji wa bidhaa na malighafi, TEHAMA, umeme, makazi, mawasiliano, ulinzi, usalama kazini, usafi, chakula n.k. Kwa upande wa makampuni ya kin-geni yamejikita katika usambazaji na utengenezaji wa mfumo mzima wa vifaa teknolojia vinavyotumika katika ujenzi wa reli ya kisasa.

Inaendelea Uk. 09

USHIRIKI WA MAKAMPUNI YA WAZAWA KATIKA UJENZI WA RELI YA KISASA - SGR

Na Mwandishi wetu TRC



“Kampuni za wazawa zaidi ya 600 zinafanya kazi katika Mradi wa SGR”



Aidha, ushirikiano wa kampuni za wazawa na Kampuni kutoka nje ya nchi umekuwa na faida kubwa katika uchumi wa nchi lakini pia katika jamii ya watanzania wakati wa utekelezaji. Hata hivyo kampuni za wazawa zimekuwa zikitoa fursa mbalimbali kama vile kuajiri wafanyakazi na vibarua, kuongeza pato la taifa na kushiriki katika kubuni, kufadhili, kufanya kazi, na kutunza mradi, kutoa ushauri katika mchakato mzima wa ujenzi ili kuhakikisha mradi unajengwa kwa kiwango kinachotakiwa na kumalizika kwa wakati.

Sambamba na dhamira kubwa ya ushirika huo wa Kampuni za ndani na nje bado tunaendelea kuona kuwa ujenzi wa reli umeinua na kukuza sekta mbalimbali kupitia Kampuni zinashiriki katika ujenzi ambapo Kampuni za wazawa

zimeweza kuzalisha ajira kwa watanzania, kuongeza uzalishaji, kukuza ujuzi pamoja na kuchangia pato la taifa kwa kulipa kodi.

Vile vile Kampuni 70 kutoka nje ya nchi zimeleta fursa ya ujuzi kwa watanzania ambapo watanzania wanapata ujuzi ambao pindi mradi utakapokamilika utawawezesha kuendesha shughulia kila siku za usafiri wa reli hii ya kisasa pia Serikali inaendelea kupata mapato kupitia kodi kwa bidhaa zinazotoka nje. Ushirikiano wa Kampuni za umma na Kampuni kutoka nje umekuwa na lengo la kuhakikisha mradi wa SGR unamalizika kwa wakati, kwani zipo kampuni za wazawa ambazo inashiriki moja kwa moja katika ujenzi wa reli katika hatua mbalimbali ikiwemo ujenzi wa tuta, Madaraja, Makalavati na hata kazi za umeme, maji n.k.

Licha ya ushirika huo vilevile Kampuni hizo zinatoa suluhisho bora wakati wa ujenzi kutokana na kwamba kila mmoja wao hufanya kazi vizuri zaidi kwa ufanisi ili kujijengea ubora na uaminifu katika kazi yake.

Tunatambua kuwa ujenzi wa reli ya kisasa ni uwekezaji mkubwa ambao unatumia gharama kubwa, hivyo serikali ililitazama hili kwa maono mapana zaidi na kuamua kuwepo na kiasi kikubwa cha ushiriki wa Kampuni za wazawa na wazawa wenyewe kama wataalamu, wafanyakazi na vibarua ili kuhamisha ujuzi utakaosaidia nchi katika siku za baadae. Aidha, kwa kutumia ushiriki wa Kampuni nyingi za wazawa Serikali imeweza kutumia fedha kidogo zaidi na kuokoa kiasi kikubwa cha fedha kwa ajili ya shughuli nyingine za maendeleo ya nchi.



SHIRIKA LA RELI TANZANIA
Mtaa wa Reli/Barabara ya Sokoine
S.L.P 76959
Dar es Salaam
TANZANIA
Barua pepe; info@trc.co.tz
Tovuti; trc.co.tz
Simu ya Bure; 0800 110 042

Limeandaliwa na Kitengo cha Uhusiano
SHIRIKA LA RELI TANZANIA
MHARIRI MKUU Jamila Mbarouk
MHARIRI MSAIDIZI Sami Omary
MTAYARISHAJI Sami Omary
MAKALA Aziza Charles
HABARI Tracylinda Nganga
PICHA Seleman Kadiko
KIBONZO Hassan Said

     [tzrailways](#)  [TRC Reli TV](#)

Reli Yetu | Maendeleo Yetu | Taifa Letu #TRCMpya